RISALA YA MKUU WA WILAYA YA MUHEZA KWA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA HAFLA YA UCHANGIAJI UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA MUHEZA KATIKA UKUMBI WA GOLDEN TULIP – DAR ES SALAAM TAREHE 16-03- 2018

Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**,**
Mhe Suleiman Jaffo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI,
Mhe.Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto,
Mhe. Ali Dovitoglu, Balozi wa Uturuki Nchini Tanzania,
Mhe Martine Shigela, Mkuu wa Mkoa wa Tanga,
Mhe. Mama Janeth Magufuli,
Mhe. Mama Marry Majaliwa,
Wahe. Mawaziri wote mlioko hapa,
Wahe. Wakuu wa Mikoa mliopo hapa,
Viongozi wa Serikali na Vyama vya siasa,
Viongozi wa Mashirika ya Serikali na yasiyo ya kiserikali,
Wadau wote wa maendeleo,
Wana Muheza wote,
Waandishi wa habari,
Mabibi na mabwana,

HABARI ZA JIONI.

Mhe, Makamu wa Rais,
Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kuwepo mahali hapa kwa wakati huu. Aidha nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii ya uchangishaji fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Muheza tunakushukuru sana.
Kwa dhati kabisa nawashukuru wageni waalikwa wote kwa ujumla wao kwa kusitisha ratiba zao na kuwa hapa pamoja nasi. Kwa heshima na taathima, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Muheza nawakaribisha wote katika hafla hii tujisikie kama tupo Muheza. **KARIBUNI SANA.**

Mhe, Makamu wa Rais,
Wilaya ya Muheza imeanzishwa mwaka 1974 ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 1,974. Wilaya ina Tarafa 4, Kata 37, Vijiji 135 na Vitongoji 522. Kwa mujibu ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Wilaya ina wakazi 204,461 na makadirio ya mwaka 2017 yanaonesha kuwa Wilaya ina wakazi 230,367 kwa ongezeko la 1.1% wakati kiwango cha uzazi ni 9.544.

Mhe, Makamu wa Rais,

Tangu Wilaya hii ianzishwe miaka 45 iliyopita haikuwahi kuwa na Hospitali ya Wilaya ya Serikali. Huduma za kitabibu kwa jamii zinapatina katika vituo vya afya na zahanati vijijini, ambapo Wilaya ina vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali 37 ikiwemo vituo vya Afya 2 na zahanati 35. Kwa kushirikiana na Taasisi binafsi vipo vituo vya kutolea huduma za afya 12 ikiwemo vituo vya afya 2, zahanati 9 na Hospitali 1 Teule ambayo inamilikiwa na Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Tanga. Kanisa la Anglikana na Serikali wameingia mkataba wa kuwapatia wananchi huduma za afya. Kwa kuzingatia ongezeko la watu na aina ya huduma zinazohitajika hospitali hii imekuwa haina uwezo wa kutosheleza mahitaji ya Wilaya kwani uwezo wake ni kuhudumia wananchi 150000 (laki moja na nusu) wakati wilaya ina wakazi 230,367(laki mbili na thelathini mia tatu sitini na saba). Hivyo huduma za rufaa ikijumuisha wagonjwa wenye hali mbaya za kiafya kutoka vituo vya huduma za msingi wanasafirishwa umbali unaofikia kilomita 72 kwenda Bombo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga. Wananchi wa Muheza wamenituma nikueleze kuwa hali hii ni tatizo kwao, hasa ikizingatiwa huduma ya afya ni kuokoa uhai wa mtu.

Mhe, Makamu wa Rais,

Wilaya yetu imedhamiria kuboresha na kuongeza uwanda wa utoaji wa huduma za kitabibu na afya kwa jamii ili kuwa na jamii yenye afya bora inayoweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali, kukuza uchumi na kuboresha hali za kijamii. Tumeazimia kuongeza utoaji wa huduma za dharura na za haraka za wanawake wajawazito, uzazi salama na watoto kutoka 1% mwaka 2017 hadi 10% ifikapo 2020, hivyo kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka 5 kutoka vifo 66 mwaka 2017 hadi vifo 40 ifikapo 2020 na vifo vya uzazi kutoka 7 mwaka 2017 hadi 3 ifikapo 2020.

Haya yote tumeona hayawezi kutimia bila ya kuwa na hospitali ambayo itakuwa chini ya uongozi na usimaizi thabiti wa Serikali.

Mhe, Makamu wa Rais,

Kwa moyo mmoja Viongozi na Wananchi wa Wilaya ya Muheza tumeamua kwa pamoja kujenga hospitali ya Wilaya kwa kujitolea kwa hali na mali na kushirikiana na Serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya Wilaya.

Ujenzi wa Hospitali hiyo unafanyika katika Kijiji cha Tanganyika, Kata ya Lusanga, Tarafa ya Muheza. Eneo la ujenzi lililotengwa ni ekari 100 ambalo limetolewa bila malipo yoyote na Kampuni ya Agrotanga mmiliki wa Shamba la mkonge la Muheza Estate. Kampuni hii inastahili pongenzi nyingi.

Ujenzi wa mradi huu unajumuisha majengo 22 ambayo yatatoa huduma zote stahili kukidhi viwango kwa Hospitali za Wilaya.

Gharama za ujenzi kwa majengo yote, samani na vifaa tiba ni Tsh. 11,322,459,300.00 **(Bilioni kumi na moja milioni mia tatu ishirini na mbili, mia nne hamsini na tisa elfu mia tatu).** Wilaya inategemea kupata fedha za ujenzi kutoka vyanzo vyake vya ndani,

kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo. Hadi sasa fedha taslimu Tsh. 40,163,837.63 **(milioni arobaini mia moja sitini na tatu elfu mia nane thelathini na saba na senti sitini na tatu)** na vifaa vyenye thamani ya Tsh. 43,415,000.00 **(milioni arobaini na tatu mia nne kumi na tano elfu)** vimechangwa na Wanamuheza na wadau wengine. Wilaya imetenga katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2018/2019 kiasi cha Tsh. 150,000,000.00 **(milioni mia moja hamsini)** za mapato ya ndani na kuwasilisha maombi ya Tsh. 2,000,000,000.00 (**Bilioni mbili**) Serikali Kuu. Aidha, maombi mengine yamepelekwa kwa wadau mbalimbali ili kufanikisha malengo.

Tunaiomba Serikali Kuu, kuweka katika mipango yake ili kutupatia fedha katika bajeti zijazo na mara ujenzi utakapokamilika iweze kutupatia wataalamu, madawa na vifaa.

Mhe, Makamu wa Rais,
Mradi unategemewa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2017/18 hadi 2019/2020, mradi utatekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza itahusisha majengo ya utawala, wodi ya wanawake, wodi ya watoto, jengo la upasuaji, jengo la maabara, jengo la utakasaji vifaa na jengo la dharura ambayo yatagharimu Tzs. 3,389,127,800.00 **(bilioni tatu milioni mia tatu themanini na tisa mia moja ishirini na saba elfu mia nane**). Uzinduzi wa kazi za ujenzi umefanyika tarehe 28/12/2017 na hivi sasa ujenzi wa majengo ya wodi ya wanawake na wodi ya watoto upo hatua ya umwagaji zege la msingi.

Lengo letu la leo ni kukamilisha majengo ya huduma za wagonjwa wanje (OPD), jengo la upasuaji, wodi ya wanawake na wodi ya watoto, hivyo tunawaomba wadau kutuchangia kiasi cha Tsh. 1,500,000,000.00 **(bilioni moja milioni mia tano)** ili huduma zianze mapema kwa kadri iwezekanavyo.

Mhe, Makamu wa Rais,
Tunaahidi kwamba, fedha na vifaa vyote vitakavyochangwa kwa ajili ya mradi huu vitatumika kwenye mradi husika na kwa uangalifu ili kupata matokeo tarajiwa. Aidha sote kwa umoja wetu tutafanya kazi kwa juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa ili kukamilisha kazi hii kwa viwango na thamani ya fedha.

Tuko tayari kusikiliza na kufuata maelekezo kutoka ngazi mbalimbali kwa nia ya kufikia azma yetu, ambayo inatupelekea kutimiza wajibu wetu katika kuwatumikia wananchi tukiwa na kaulimbiu yetu ***"MUHEZA MAENDELEO MBELE, HAKUNA KULALA HAPA KAZI TU"***

Mhe, Makamu wa Rais,
Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wale wote waliofanikisha hafla hii, Naomba mpokee shukurani zetu za dhati, kwanza kwako wewe Mheshimiwa Mgeni rasmi na waalikwa wote waliofika mahali hapa. Shukurani za dhati ziwaendee wadau wote waliojitolea kutuwezesha kuwepo mahali hapa wakati huu, wakiwemo kampuni ya MAXCOM waliodhamini utengenezaji wa namba za uchangiaji, Uongozi wa Golden Tulip,

Propel production, Tunkey architect, Pembe Flour Mills Ltd, Hugodomingo design, kampuni ya Said Salim Bakharesa, TSN, vyombo vya habari, pamoja na wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha shughuli hii. Kwa uhakika sipati maneno mazuri au mahususi yanayoendana na thamani ya mliyotutendea. Zaidi nasema ASANTENI SANA NA MBARIKIWE NA MUNGU.

Tunawaomba viongozi wetu, wadau wetu, ndugu zetu na marafiki zetu popote walipo kuunga mkono juhudi hizi. "***JENGA HOSPITALI OKOA MAISHA"***

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA

NAOMBA KUWASILISHA